

Nafasi ya Fasihi - Mazingira Kuelekea Uchumi wa Viwanda Nchini Tanzania: Mifano Kutoka Katika Nyimbo za Mrisho Mpoto na Beka Flavour

**By
Rose Sekile**

Chuo Kikuu Katoliki Mbeya
rosesekile80@gmail.com

Ikisiri

Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Data za msingi zilipatikana katika jamii kwa kuchunguza nyimbo zinazohusu mazingira. Mbinu ya usomaji makini na upembuzi yakinifu zilitumika kupata data za msingi. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Ekolojia ndiyo iliyoongoza katika mjadala wa uchanganuzi wa data zilizowasilishwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya mazingira na uendelezaji wa viwanda. Aidha, nyimbo ni nyenzo muafaka ya kuelimisha jamii kuhusu utunzaji wa mazingira na kudhibiti mienendo na tabia isiyofaa katika jamii. Utunzaji wa mazingira nchini Tanzania inaonekana ni jukumu la asasi zilizopewa dhamana kuhusu mazingira na si jukumu la kila mmoja wetu. Makala haya yanapendekeza kuwa ni vyema uelimishaji wa elimu mazingira ufanyike katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya kaya hadi kitaifa ili kumfanya kila mmoja wetu awe sehemu ya utunzaji wa mazingira. Uanzishwaji wa viwanda na ukuaji wa uchumi unatakiwa uende sanjari na uhaishaji wa mazingira.

Istilahi muhimu: Mazingira, Fasihi - mazingira, ekolojia, uchumi na uchumi wa viwanda

1.0 Utangulizi

Makala haya yanachunguza nafasi ya fasihi - mazingira kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Thirmurthy (2004) anasema kuwa mazingira ni vitu vyote vilivyo hai na visivyo hai vinavyomzunguka binadamu. Aidha, anaendelea kufafanua kuwa mazingira ni pamoja na maliasili zinazopatikana katika maeneo tunayoishi, hewa, ardhi na maji, uhai wa mimea na wanyama, hali ya kijamii, pamoja na kiuchumi. Mambo mengine ni hali inayoshawishi maisha ya binadamu na jumuiya zao, majengo, miundo-mbinu, mitambo na mambo mengine yaliyoundwa na wanadamu, mada ngumu, vimiminika, joto, sauti, mitetemo, mnururisho wa moja kwa moja na ule unaotokana na shughuli za kibinadamu au mchanganyiko wa mahusiano ya vyote vilivyotajwa hapo juu. Fasihi- mazingira ni uwanja unaojadili dhana ya kimazingira katika fasihi na sanaa nyingine. Uwanja huu unachukua mkabala wa wahusika wanavyohusiana na ekolojia, maudhui ya ekolojia na jinsi lugha inavyovyazwa na ekolojia.

Pia, ni maandiko ya kitaalamu yanayoeleza kuhusu maudhui yahasu mazingira, hususani yanayofafanua mahusiano yaliyopo kati ya binadamu, jamii na mazingira. Payne na Barbara (2010) wanasema kuwa uwanja huu unachukua mwelekeo wa kimwingiliano taaluma kwa

kuhusisha usomi wa mandhari, nyanda na sehemu za dunia kuoanisha na sanaa mbalimbali. Fasihi- mazingira katika Fasihi huchunguza na kutalii uhusiano uliopo kati ya matini ya kifasihi na mazingira asilia, maarubu ya mazingira asilia katika vitushi vya sanaa. Thamani ya kimazingira anayowasilisha msanii endapo inawiana na maarifa ya kiikolojia na inachunguza tofauti za kimazingira za sanaa za mwanaume na mwanamke. Pia, inachunguza athari za fasihi - mazingira kwa hadhira yake na namna mazingira yanavyojipenyeza katika fasihi. Mwisho, inachunguza mwingiliano unaojitokeza baina ya masimulizi ya mazingira, mapisi, falsafa, maadili, saikolojia, anthropolojia, utamaduni na fasihi (Nabeta, 2014). Kazi zenye mlengo huu, hujadili pia namna ujumi wa kifasihi uliomo kwenye kazi za fasihi unavyodhihirisha jinsi tamaduni za jamii zinavyoimba kudhibiti na kuukilia mitazamo, imani, elimu, na ufahamu kuhusu mazingira.

Ekolojia ni taaluma inayochunguza kuhusu mifumo na dhana ya maumbile kiasilia. Dhima ya mifumo ya ekolojia huathiriana na jinsi binadamu anavyohusiana na mazingira yake (Odun, 1971). Pia, ni sayansi inayochunguza uhusiano uliopo kati ya viumbe hai na mazingira wanayoishi. Ekolojia inajaribu kutabiri mabadiliko yanayohusiana na shughuli za wanadamu. Duniani kote, tafsiri pana ya viwanda inajumuisha uchimbaji wa madini na mawe, utengenezaji wa bidhaa na huduma za uzalishaji na usambazaji wa maji, usimamizi wa maji taka, taka nyingine na shughuli za kurekebisha uharibifu wa mazingira na ujenzi. Ujenzi wa uchumi wa viwanda ni kufanya mageuzi ya kimfumo, kijamii na kiuchumi yanayotawaliwa na teknolojia na kuongeza uzalishaji yanayofanya viwanda kuchangia zaidi katika ukuaji uchumi. Maendeleo ya viwanda yanachangia sana uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Uanzishaji wa viwanda ni jambo zuri ili kufikia uchumi wa thabiti, ingawa hatua makini zisipotekelzwa kwa uangalifu linaweza kuharibu mazingira na uhai wa viumbe hai. Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania.

2.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania. Data za msingi zilipatikana katika jamii kwa kuchunguza nyimbo zinazohusu mazingira. Mbinu ya usomaji makini na upembuzi yakinifu zilitumika kupata data za msingi. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Ekolojia ndiyo iliyoongoza katika mjadala wa uchanganuzi wa data zilizowasilishwa. Nadharia ya Ekolojia iliasisiwa na Glotfelty (1995) nchini Marekani. Ajenda kuu ya nadharia hii nikuyachunguza na kushughulikia masuala yanayohusiana na mazingira. Mara nyingi matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zinatokana na shughuli za kibinadamu. Hali hii inatokea pale shughuli za kibinadamu zinapoharibu uwezo wa kawaida wa dunia kuwezesha uendeleu wa mifumo ya ekolojia. Pia, inahusika na dhima ya mazingira katika kuukilia utamaduni wa jamii katika kipindi mahususi cha kihistoria, pamoja na mila na desturi zinazohusishwa au

zisizohusishwa na hali ya mazingira. Katika makala haya nadharia hii imetumika kuichunguza nafasi ya fasihi katika kuendeleza uchumi wa viwanda nchini Tanzania.

Pia, nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa karne ya 19 na kufafanuliwa zaidi na Goffman (1952), Hegel (1971) na Lukacs (1979). Uhalisia unasisitiza zaidi usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Wanauhalisia wanaona kwamba kazi ya fasihi inapaswa kuwa sahihi, iliyo wazi na inayozingatia masuala halisi bila ya kupiga chuku. Wanauhalisia wanasema kuwa msanii anapaswa kuteua, lakini akiwa na nia ya kuendeleza masuala yake kama yanavyowahusu watu katika hali halisi za maisha. Katika makala haya, nadharia hii imetumia kuchunguza uhalisia wa mazingira ya sasa na jinsi yanavyosawiriwa na mtunzi sambamba na maudhui yake. Pia, imechunguza na kudhihirisha ukweli wa kile alichokisawiri mtunzi anapochunguza uhusiano wa asahi na mazingira.

3.0 Uwasilishaji na Uchambuzi

Makala haya yamechunguza nafasi ya fasihi mazingira katika kuelekea uchumi wa viwanda nchini Tanzania kwa kurejelea nyimbo za Mrisho Mpoti na Beka Flavour. Makala haya yamechunguza uhusiano wa nyimbo na mazingira asilia, taswira halisi ya mazingira katika nyimbo na mchango wa nyimbo katika utunzaji wa mazingira na kuinua uchumi wa viwanda kama ilivyoielezwa katika sehemu inayofuata.

3.1 Uhusiano wa Nyimbo na Mazingira Asilia

Fasihi kama taaluma ina uhusiano wa kiutegemezi au kiutegemeano na mazingira. Fasihi hususani nyimbo hutumia vitu mbalimbali vilivyo katika mazingira kufikia dhima yake. Msanii anaposana kazi yake hupata maarifa kutoka katika mazingira. Nyimbo ni nyenzo muafaka inayotekeleza mambo yanayotokana na msukumo wa hali halisi ya maisha. Hegel (1971) anasema kuwa kazi ya fasihi inatakiwa kutekeleza mambo kutokana na msukumo wa hali ya maisha wanamoishi. Mtunzi anatakiwa atoe usimulizi ambao unajikita katika kusimulia ukweli unaofahamika katika maisha ya binadamu. Hakuna sanaa inayojipambanua nje ya maisha ya mwanadamu, hata kama ikitokea maudhui yake yakawa katika historia ya mambo yaliyopita, sharti yatafumuwa katika fani inayopambanua maisha halisi (Okpewho, 1992). Fasihi ni uhalisia unaotokana na shughuli za binadamu ambazo hufanywa kila siku na matukio ya kweli na yenye uhalisi. Binadamu ndio wanaoshiriki katika shughuli za kila siku katika maisha na maendeleo ya jamii. Beka Flavour katika wimbo wa '*Mazingira*' anaeleza:

Kuyatunza mazingira ni wajibu wa kila Mtanzania,
Tena bila kufosiwa, majumbani tunamoishi wenyewe,
Tuelimishane kuhifadhi mazingira, vyanzo vya maji tuvilinde,
Tuviheshimu na tuvitunze, tuvipende hivyo ni vitu muhimu,
Na baharini tusiende kutupa takataka, samaki waringe nyumba,

Yao ya maisha, wavuvi pia mjifunze kuacha uvuvi haramu, mabomu,
Ya nini kwenye maji kama mna vita na Vietnam na viwandani chonde,
Chonde moshi huharibu mazingira na maji taka vile vile si mazuri,
Kwetu binadamu, tutapiga hatua tukiungana kuyatunza mazingira.

Binadamu ana uhusiano na mwingiliano mkubwa na mazingira yake. Uhusiano huo unaweza kuwa wa binadamu na binadamu mwenzake, wanyama na mimea. Uhusiano huu unaweza kuwa wa kijiografia kama vile misitu, mito na mabadiliko ya hali ya anga. Pia, unaweza kuwa mazingira ya kijamii kama vile shule, familia, ujirani na utamaduni. Uhusiano huu unachangia sana katika ukuaji na uendelezaji wa uchumi. Katika uhusiano, upatano na mwingiliano huu binadamu ndiye ana athari kiuchumi, kisiasa na kijamii, tofauti na viumbe vingine vyote. Odun (1971) anasema kuwa dhima ya mifumo ya ekolojia huathiriwa na jinsi binadamu anavyohusiana na mazingira yake. Tamaduni za jamii zina athari chanya au hasi kuhusu uhai wa mazingira na uchumi kwa jumla. Glotfelty (1996) anasema kuwa vitendo vinavyohatarisha maisha ya binadamu vinaweza kujengewa misingi yake kutegemeana na utamaduni wa matumizi ya mazingira asilia.

Ulimwengu umezungukwa na mambo mengi yanayosababisha uchafuzi wa mazingira. Binadamu anapoendelea kuhitilafiana na mazingira yake huathiri maendeleo yake kiuchumi, kijamii na kisiasa ambayo huibuka kila siku. Kutokana na uharibifu wa mazingira katika karne hii ya ishirini na moja, binadamu anatakiwa kuibuka na mbinu mpya za kutunza mazingira ya kiasili na jinsi ambavyo anastahili kuingiliana nayo (Claser, 2002). Ili binadamu ajielewe na kufikia uwiano kati yake na mazingira anamoishi, lazima ajielewe na kujitambua. Fasihi humfanya mtu aelewe mazingira anamoishi. Fasihi yoyote ile haikosi kufundisha jambo kimakusudi ama kisadfa. Fasihi inachora taswira ya uhalisi wa maisha ya binadamu na mazingira; na kuwasilisha hali, maingiliano, mivutano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Ntarangwi (2004) anasema kuwa kazi ya fasihi inafaa kuwaweka wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi.

3.2 Taswira Halisi ya Mazingira katika Nyimbo

Taswira ni picha ya mambo au vitu inayomjia mtu akilini mwake (TUKI, 2004). Msanii ana zana zake anazitumia kuchora taswira akilini mwa mtu. Zana hizo ni uhodari wa maneno yanayopangiliwa kwa utaratibu ambao huleta mguso na mnaso kwa msikilizaji. Lugha iliyojaa usanifu, urazini na umahiri ambao ndicho chombo maridhawa cha fasihi kinachotumika kutoa ujumbe wa fanani kwa hadhira. Mazingira katika fasihi ni kitu chenye maana na umuhimu katika utunzi wa kazi ya sanaa. Msanii anapobuni kazi yake hutumia vitu vilivyomo kwenye mazingira. Vitu hivyo ndivyo hutumika kujenga taswira katika akili ya mtu (Escarpit, 1974). Ubunifu huo hufanyika wakati msanii anataka kutoa lile alitakalo ambao ulikuwa unamkereketa moyoni mwake. Senkoro (2011) anasema kuwa inategemea wahusika hao

wanawakilisha nini na wanatumiwaje katika kazi za fasihi. Sanaa yoyote inachipuka kutokana na mila na desturi zilizo katika mazingira aliyomo mtu. Fasihi simulizi lazima ichukuliwe kama ilivyo na uhusiano usiotatanika na maisha ya jamii.

Wasanii wengi, wakiwemo watunzi wa nyimbo kwenye kazi zao wanaeleza kile wanachokishuhudia kwa sasa kuhusu uharibifu wa mazingira. Sanaa zao zimeweka juhudi za wahusika kuvaa uhusika wa harakati za kutetea uharibifu wa mazingira (Njogu na Chimera, 1999). Msanii hupata msukumo wa kutunga kazi yake kutokana na matukio na mabadiliko yanayoikumba jamii katika mazingira wanamoishi. Hegel (1971) anauona ulimwengu mzima kama unaoelewa kwa kueleza na kusimulia mawazo ya kweli ambayo yanapatikana katika ulimwengu wa kihalisia. Nyimbo hazina budi kuchangia na kutoa msukumo zaidi kuchangia masuala ya kimazingira, kwa kuwa hufungamanishwa na maisha ya binadamu. Kwa mfano, wimbo wa msanii Mrisho Mpoto ulioimbwa kwenye kampeni ya mazingira ‘*Nitunze Nikutunze*’ ulitoa taswira halisi ya mazingira yetu ya sasa. Kampeni hii ilifanyika Mbagala, jijini Dar es Salaam. Kampeni hii ilikusanya watu wengi, wengi wao wakitaka kumuona msanii huyo. Ujumbe ambao aliutoa kwenye wimbo huu uliwavutia watu, wakavutika na kushiriki kuimba wimbo huo. Wimbo uliwahamasisha wananchi wainuke, wacheze nawafurahi, lakini msititizo ulikuwa ni utunzaji wa mazingira. Taswira na maneno yaliyomo ni yale yaliyo katika mazingira. Taswira iliyojengwa akilini mwao ni ya vitu walivyonyavyo, wanavyoviona na kuvishuhudia katika maisha yao halisi. Katika ubeti wa pili anasema:

Hebu angalia mashoka yanavyoangusha miti na kuacha ardhi uchi bila marejesho,
Wale wanyama wanaozurura kutafuta malisho ndiyomaendeleo?
Ile mioshi inayokeshwa kila kukicha katika anga ndiyomaendeleo?

Jambo la kawaida kuona viumbe hai wamehama katika mazingira yao asilia kutokana na uharibifu wa makazi yao ya awali, chanzo kikubwa kikiwa ni binadamu. Baadhi ya jamii hupenda kuchoma moto, kulima, kuanzisha shughuli za uzalishaji mali kama vile viwanda vikubwa na vidogo. Utafiti huu umebaini kuwa binadamu anapotumia teknolojia ya kisasa wakati anazalisha bidhaa viwandani, anahitilafiana na mfumo wa ekolojia. Kwa mfano, moshi unaotoka viwandani unaharibu hewa inayotumiwa na wanyama, binadamu na hata mimea. Serikali inatakiwa kuwa na mikakati madhubuti wakati wa kuanzisha viwanda ili kuhakikisha havitoi kemikali zenye sumu ambazo zinaweza kuhitilafiana na mfumo wa ekolojia. Msanii anahoji ile mioshi inayokeshwa kila kukicha katika anga ndiyo maendeleo? Tabia ya kutojali thamani ya mazingira inapaliliwa na tamaduni zisizojali uendelezaji wa mazingira. Utamaduni wa jamii unaweza kuchochea uendelevu wa mazingira au uharibifu wa mazingira. Msanii anasema hebu angalia mashoka yanavyoangusha miti na kuacha ardhi uchi bila marejesho. Wananchi wanatakiwa waelimishwe na washauriwe kuhusu mazingira ili taifa liweze kufikia lengo la uchumi wa viwanda.

3.3 Nyimbo katika Kuendeleza Mazingira na Kukuza Uchumi wa Viwanda

Kipury (2000) anasema kuwa nyimbo, lazima zitumike kuichambua na kuelezea falsafa ya maisha ya jamii ya watu, utamaduni, historia na maendeleo ya jamii hiyo. Watunzi wengi wa kazi za fasihi huyatumia mazingira ya kijiografia kuonesha jinsi binadamu anavyoweza kuingiliana na mfumo wa ekolojia. Mtazamo wa wana-ekolojia unamakinikia sana uhusiano baina ya binadamu na mazingira asilia. Mara nyingi, matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zitokanazo na shughuli za kibinadamu. Wamitila (2008) anasema kuwa mandhari ya kijiografia ni nguzo muhimu sana katika uchunguzi wa kazi ya fasihi hasa zile zilizoandikwa katika mkondo wa kihalisia. Nyimbo ni njia muafaka inayoweza kudhibiti mienendo, tabia, na matendo yasiyofaa katika jamii kwa sababu hukaririwa kwa urahisi. Njiru (1981) anasema kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi na amali za jamii. Fasihi mazingira inazidi kuchukua dhima mpya katika jamii kadri inavyozidi kukua kiteknolojia, ingawa dhima ya kazi za kifasihi katika jitihada za kutunza mazingira haijapewa uzito kitaaluma. Pengine, yanachukuliwa kama masimulizi yasiyo na uwezo na mashiko katika kushughulikia utunzaji wa mazingira (Ogechi, 2015). Ujumbe uliomo katika kazi za fasihi kuhusu usawiri wa mazingira, ufundishwaji na uhakiki wa kazi za fasihi simulizi kuhusu utunzaji wa mazingira ni wa muhimu sana katika kuitanabisha jamii kuhusu mazingira.

Masuala ya kiuchumi, kwa kiasi kikubwa, hushikiliwa na viongozi waliopewa dhamana na wananchi. Viongozi hawa ndio huweka sainsi kwenye mikataba ya wawekezaji bila kuzingatia suala la uhifadhi wa mazingira; huongoza mifumo ya kiuchumi na nyenzo za kuzalisha mali katika jamii. Katika ubeti wa nne anasema ‘Wizara yako ndiyo wizara mama ambayo tunaitegemea, ndiyo inashika mhimili wa nchi yetu. Tumia sauti yako mheshimiwa Waziri, tumia kalamu yako, tumia nafasi yako’. Katika utekelezaji wa mikataba ya uanzishwaji wa viwanda, viongozi wenye dhamana hawazingatii sana mfumo wa ekolojia ambao ni mfumo wenye tija katika uendeshaji wa viwanda na ukuzaji wa uchumi. Wimbo huu unaeleza namna ongezeko la watu linavyohusiana sana na uharibifu wa mazingira. Wanaikolojia wanasema kuwa, mara nyingi, matatizo ya kimazingira yanayowasilishwa katika kazi za fasihi yanachukuliwa kuwa ni athari zitokanazo na shughuli za kibinadamu. Bronfenbrenner (2005) anasema kuwa maendeleo ya binadamu ya kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiutamadunina kiteknolojia huathiriwa na jinsi ambavyo anaingiliana na mazingira anamoishi. Mifumo ya kiuchumi, hususani uanzishwaji wa viwanda, umekuwa na changamoto kubwa sana katika uhuishaji wa mazingira. Mfumo huu wa kiuchumi unahujumu sana mfumo wa ekolojia jamii kwa sababu hauzingatii suala la mazingira.

Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania (MKUKUTA) unatambua kuwa mazingira bora ni muhimu kwa kuleta maendeleo endelevu. Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 imeeleza wazi wajibu na majukumu ya wadau mbalimbali, kuanzia serikali za mitaa hadi taifa,

kuhusu usimamizi wa matumizi endelevu ya mazingira, kudhibiti uchafuzi wa mazingira , utunzaji wa taarifa na takwimu za mazingira, utafiti na ushiriki wa jamii katika kutekeleza mikataba. Jamii yoyote hujijengea moyo wa kuthamini misingi ya utu, usawa, upendo, na usalama wa mazingira yake. Hivi sasa uelewa wa jamii kuhusu masuala ya mazingira umepewa kipaumbele katika kuandaa mipango ya maendeleo, ingawa jamii haina taarifa za kutosha kuhusu elimu – mazingira, hivyo basi nyimbo zitumiwe kufikisha taarifa hizo kwasababu ndizo huweza kuwafikia watu kwa urahisi na wepesi.

3.4 Mchango wa Nyimbo katika Utunzaji wa Mazingira na kuinua Uchumi wa Viwanda

Nyimbo ni mkufunzi ni mwalimu wa Fasihi mazingira. Mazingira yanahusishwa moja kwa moja na uhai wa binadamu na uhai wa taifa kwa jumla. Uchumi wa taifa unategemea sana uhai wa mazingira; hata vipengele vingi vya maisha ya mwanadamu vinategemea uhai wa mazingira. Katika jamii ya sasa, wanajamii wanasaka utajiri, huku wakiharibu mazingira yanayowatunza. Maarifa ya elimu - mazingira yanatakiwa yaelezwe kwa jamii kwa namna ambayo ni ya kawaida kwa kutumia elimu-jamii, hususan nyimbo. Katika kuelimisha jamii, mara nyingi nyimbo zinazoimbwani zile zenye mafumbo, sitiari na ishara ambazo ziko katika mazingira yao. Msanii anatumia jazanda zilizosheheni sitiari na udokezi wa kijadi unaoonesha maarifa na uelewa mkubwa wa utamaduni unaohusika. Kwa mfano, kwa kutumia nyimbo zenye mizaha na kebehi, watu hujifunza, hufurahishwa, na kuchekeshwa, hasa katika mikusanyiko isiyo rasmi kwenye jamii. Mara nyingi, njia ya kejeli au kebehi huwafikia watu kwa urahisi zaidi. Jamii ina namna yao ya kuwasiliana, yaani kutumia lugha yao ya kawaida waliyozoea kuwasiliana na ambayo nyingi, si lugha rasmi.

Uchafuzi na uharibifu wa mazingira ni matokeo halisi ya jamii lengwa. Jamii isiyotunza mazingira inahatarisha kizazi kijacho, na athari hizi huenda zikaonekana miaka mingi baadaye. Katika muktadha huu, tumebaini kuwa nyimbo zinazoimbwa na makundi maalum katika jamii zina mchango mkubwa sana katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira ili kuweza kufikia uchumi wa kati. Nyimbo hizo zimekuwa chachu katika uendelezaji wa mazingira. Heise (2008) anasema kuwa fasihi, hususani nyimbo zina uwezo wa kujenga utamaduni utakiwao kuhusu utunzaji wa mazingira wenye manufaa kwa binadamu na viumbe wengine. Hivyo, ni makosa kuamini kuwa sayansi pekee ndiyo inayoweza kutatua suala la utunzaji wa mazingira. Fasihi ina wajibu wa kuchora jamii kama ilivyo na ni muhimu kuyaeleza mambo yaliyopo ili kuwafungua macho na kuwapevusha wanajamii. Mbinu ya kutumia nyimbo kuisitiza maudhui ni ya asili, kwani imekuwa ikitumika kwa muda mrefu katika masimulizi ya kijadi. Njia hii imetumika pia kwa miaka mingi kukaririsha watoto maarifa mapya na kuhakikisha kuwa maarifa hayo hayasahauliki kwa urahisi. Uzalendo wa mazingira unatakiwa upandwe ndani ya watoto kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu, ili wanapokuwa watu wazima wawe na maarifa yanayohusisha uzalishaji mali na utunzaji wa mazingira . Elimu si rahisi sana ikianza katika hali ya utu uzima.

4.0 Hitimisho

Fasihi mazingira ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na uendelezaji wa viwanda. Matatizo yatokanayo na tabia ya nchi yanayochochewa na uchafuzi wa mazingira na uharibifu wa mazingira yangeweza kudhibitiwa kwa kutumia mafunzo ya elimu inayopatikana katika Fasihi simulizi, hususani nyimbo, kwa sababu Fasihi simulizi inaishi na watu, na inamgusa kila mmoja. Harakati za kijamii za uchafuzi na uharibifu wa mazingira hazijatolewa elimu ya kutosha itakayoweza kuwafanya wanajamii wenyewe wawe sehemu ya udhibiti mazingira. Mazingira yanapohitilafiwa, shughuli za uzalishaji nazo zinakwama. Shughuli za kiuchumi zinapaswa kusaidia hifadhi ya mazingira, ikiwa ni pamoja kuhakikisha kuwa mifumo ya ki-ekolojia na mahitaji ya msingi ya ustawi wa jamii vinalindwa. Pia, ukombozi wa fikra-mazingira ufanywe kupitia elimu jamii kuanzia ngazi ya kaya. Kila mmoja ajione kama sehemu ya mazingira. Ukombozi huu huanza kwa lugha ya mazungumzo, si kwa maandishi. Mulokozi (2017) anasema kuwa, inasemekana sisi Waafrika hupenda sana kuongea, labda ndiyo maana hatupendi kusoma na kuandika. Kuongea huku kwa namna ya kawaida kwa kutumia mawasiliano ya ana kwa ana hutuvutia zaidi. Wadau wote wapewe fursa ya kutoa michango na kupata mrejesho wa masuala ya mazingira, kwani yanaweza kuchochea na kusaidia changamoto katika usimamizi na utunzaji wa mazingira yao. Katika utafiti huu tumebaini kuwa kipera cha nyimbo kitasaidia kuelimisha jamii na wawekezaji kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Kwa hakika, kama zinavyodai nadharia za uhalisia na ekolojia, jamii inatakiwa ielezwe kwa uhalisi wake ili kuleta mabadiliko ya kimazingira. Watu wakila tabaka wanatakiwa kuchochewa ili kubadili fikra zao kuhusu suala zima la mazingira na ukuaji wa uchumi.

Marejeleo

- Bronfenbrenner, U. (2005). *Making Human Being Human Biological Perspectives on Human Development*. London: Sage Publications Limited.
- Claser, M. (2002). *Human and Nature Interaction in the Anthropocene Potential of Social – Ecological system Analysis*, Makala kutoka <http://www.oekm.de>.
- Glotfelty, C., & Fromm, H. (1996). *The Ecocritical Reader*. London: New York Routledge.
- Hegel, G.W. (1971). *Introduction to Aesthetics*. Clarendon: Oxford University Press.
- Heise, U.K. (2008). *Ecocriticism and Transnational Turn in American Studies*. Imechukuliwa May, 2022 katika www.muse.jhu.edu/journals/alh/summary/v020/20/heise.htm.
- Kipurry, N. (2000). *Oral literature of the Maasai*. Dar es Salaam: Ujuzi Educational Publishers.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: MoconPrinting Press.
- Njogu, K., na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo

Kenyatta Foundation.

Okpewho, I. (1992). *African Orala Literature Backgrounds, Characters and Continuity*, Bloomington and Indiana Polis: Indian University Press.

Odun, E. (1971). *Fundamental of Ecology Philadelphia*. Makala kutoka <http://www.researchgate.net>.

Ogechi I.U. (2015). Nature in Nigerian Childrens Literarure:An Appraisal of Selected Verses. Tasnifu ya Umahiri, Ahmadu Bello, Zaria.

Payne, M., &Barbara, R. (2010).*Dictionary of Cultural and Critical Theory*. Wiley: Blackwell Publishers.

Thirmurthy, A.M. (2004). *Principle of Environmental Sciences, Engineering and Management*. Mumbai: Shroff Publishers.

Wamitila, K. W. (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited.